JINSI YA KUJIBU SWALI LA VITABU (TAMTHILIYA) –KIDATO CHA 3&4

SWALI: "Wasanii wa kazi za Fasihi huangalia matatizo yaliyomo katika jamii na kuamua kutumia kalamu zao kuyaweka wazi ili kuirekebisha jamii". Thibitisha kauli hii kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma. (Toa hoja nne kila kitabu).

MAJIBU

Ni kweli wasanii huangalia matatizo yanayozikabili jamii zao na kuyaweka wazi ili jamii iweze kukabiliana nayo. Ukweli huu unathibitika kupitia tamthiliya ya KILIO CHETU pamoja na tamthiliya ya ORODHA kama ifuatavyo:

Kwa kuanza na tamthiliya ya KILIO CHETU watunzi wamebainisha wazi matatizo yanayoikabili jamii kama ifuatavyo:

Janga la UKIMWI, jamii inakabiliwa na tatizo hili kwa sababu ugonjwa huu unapoteza nguvukazi ya taifa na pia kuchochea umaskini katika, kwa mfano familia ya "Baba Joti" ilikumbwa na janga hili kwa kumpoteza "Joti" akiwa mtoto mdogo. Ili kuepukana na janga hili ni muhimu kwa jamii kutoa elimu kwa vijana juu ya madhara ya mahusiano ya kimapenzi kabla ya wakati wake.

Utandawazi, hili nalo ni tatizo kwani vijana wengi hawana uelewa juu ya matumizi bora ya maendeleo ya sayansi na teknolojia, mathalan vijana hutumia mitandao ya kijamii kuangalia picha za (x) na matokeo yake ni kuiga wanayoyaona bila tahadhari yoyote. "Joti" na kundi lake ni mfano wa vijana walioathiriwa na utandawazi wanasikika wakijisifu kutazama picha za (x) bila kuota kama walivyokuwa wakielezwa na wazazi wao. Jamii kwa ujumla inapaswa kutoa miongozo sahihi juu ya matumizi bora ya matokeo ya sayansi na teknolojia kama vile simu, kompyuta na televisheni.

Makundi rika, vijana wengi humezwa na makundi ambayo huwachochea kujiingiza kwenye matendo yasiyokubalika katika jamii, mfano "Mwarami" alishawishiwa na kundi lake kujiingiza kwenye mahusiano ambayo hayakufanikiwa kutokana na "Anna" kujitambua baada ya kupewa elimu na wazazi wake. Ni muhimu sana vijana kuelimishwa namna bora ya kuchagua marafiki na makundi ya marafiki wa kuungana nao.

Imani za kishirikina, baadhi ya watu mpaka hivi leo hawaamini juu ya kuwepo kwa ugonjwa wa UKIMWI na kuwa hauna chanjo wala tiba. Mfano ni "Jirani" ambaye anashauri "Joti" apelekwe kwa fundi huko Luhota licha ya daktari kuleta majibu ya vipimo kwamba kinachomsumbua "Joti" ni maambukizi ya virusi vya UKIMWI na hivyo mgonjwa apatiwe tiba kwa magonjwa nyemelezi, chakula bora na kuoneshwa upendo wa dhati, hii itamfanya aishi muda mrefu. Imani hizi hufanya watu kupuuza maelekezo ya wataalamu na kukatiza maisha ya wagonjwa mapema.

Malezi, hili nalo ni tatizo kutokana na wazazi wengi kutojua mbinu bora za malezi kulingana na wakati tulionao. Wapo wazazi wanaoamini kwenye viboko na vitisho kama "Mama Suzi" na "Baba Joti" lakini pia wapo wanaoamini kwenye kuwapa watoto na vijana elimu ya kujitambua kama inavyosisitizwa na "Baba Anna" na "Mjomba". Ukweli ni kwamba zama zimebadilika na hivyo mbinu za malezi nazo hazina budi kubadilika.

Kwa upande wa tamthiliya ya ORODHA mtunzi wa tamthiliya hii anabainisha matatizo yanayoisibu jamii yake kama ifuatavyo:

Janga la UKIMWI, jamii hasa vijana ni waathirika wakubwa wa janga hili kutokana na mazingira yanayowazunguka ikiwemo kutomudu mahitaji yao ya msingi kama ipasavyo, mathalan "Furaha" alijiingiza kwenye mahusiano na "Bw. Ecko" ili tu aweze kupata baadhi ya vitu vizuri ambavyo kimsingi wazazi wake hawawezi kumudu kumpatia.

Athari za makundi, baadhi ya vijana hujiingiza kwenye matendo yasiyokubalika katika jamii kwa sababu tu ya kushawishiwa na makundi waliyomo, kwa mfano "Furaha" alijiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi kutokana na ushawishi wa "Mary". Kupitia ushawishi huu sio tu kuwa "Furaha" alijiingiza kwenye mahusiano na mtu mzima sana wa kutosha kuwa baba yake lakini pia alishiriki ulevi bila ambao ulimfanya ashindwe kujitambua na hatimaye kulala na "Bw. Ecko". Vijana wanapaswa kuwa makini sana na marafiki zao.

Mmomonyoko wa maadili, hili nalo ni tatizo sana kwa sasa hasa tunapoona wazee wanashiriki mapenzi na vijana wa kutosha kuwa watoto au hata wajukuu wao, uadilifu unapotoweka huwa ni janga kwa jamii. Ukweli huu unathibitika kupitia "Padri James" ambaye anaendekeza tamaa za mwili na kuzini na "Furaha"

aliyekwenda kufanya toba kutokana na dhambi aliyoitenda. Matendo ya watu aina ya “Padri James” yanatia doa sana watumishi wa Mungu mbele ya watu wanaowaongoza.

Mapenzi na ndoa, familia nyingi hivi leo zinayumba kutokana na kupungua kwa mapenzi ya dhati baina ya wanandoa na hatimaye kuchochea usaliti. Mfano mzuri ni “Bw. Ecko” ambaye anamuacha mke wake wa ndoa na kwenda kuzini na “Furaha” mtoto mdogo. Ukosefu wa uaminifu katika ndoa huleta mifarakano ndani ya familia, watoto huteseka iwapo wazazi watatengana na pia huweza kuleta magonjwa kama UKIMWI iwapo mwanandoa mmoja atachepuka. Kukaa na kuzungumza ni suluhisho bora sana iwapo kumetokea kutoelewana baina yao.

Imani potofu, watu wanaposhikilia imani hizi husababisha mkanganyiko ndani ya jamii juu ya mambo yanayohitaji utaalamu, mathalani kitendo cha watu kuamini kuwa kifo cha “Furaha” kinachangiwa na mzimu ni dalili mbaya juu ya watu kutoamini kabisa kuwa UKIMWI upo na unaua. Lakini pia kitendo cha “Bw. Ecko” na “Bw. Juma” kuamini kuwa ukilala na msichana bikra basi unapona UKIMWI ni imani potofu na huweza kuchochea maambukizi ya virusi hatari vya UKIMWI. Jamii inapaswa kuachana na imani za namna hii kwani huwa ni kikwazo katika utoaji wa elimu kwa jamii.

Ukweli, jamii pia inakabiliwa na tatizo la kutokubali ukweli wa mambo yanayoikumba na kuiathiri jamii kutokana na kutokujua ukweli ulivyo, mfano mzuri ni “Mama Furaha” ambaye amekuwa mtu wa kwanza kushikilia kuwa ukweli lazima usemwe kwamba “Furaha” amefariki kutokana na janga la UKIMWI kitu ambacho mhusika mwenyewe anataka kifanyike ndiyo maana ameacha barua na orodha ambayo anaamini jamii ikifahamu basi itajitahidi kuchukua tahadhari stahiki. Ni dhahri kuwa ukweli ukiwekwa wazi jamii pana inaweza kuepuka matatizo yanayoweza kuepukika.

Kwa ujumla watunzi wa kazi za Fasihi hufanya kazi kubwa ya kuibadilisha jamii kupitia kalamu zao hivyo ni wajibu wa jamii kuzingatia elimu itolewayo na kuitendea kazi ili kuleta mabadiliko yanayokusudiwa na wasanii hao.